## TAARIFA KWA UMMA

# KUSITISHA RATIBA ZA MABASI 38 YA KAMPUNI YA *NEW FORCE* YANAYOANZA SAFARI SAA 9.00 NA SAA 11 ALFAJIRI

**Tarehe 3 Julai, 2023**

Kwa siku za karibuni tumeshuhudia ajali za mabasi ya abiria ya masafa marefu ambazo zimesababisha madhara madogo na makubwa kwa abiria. Ndani ya takribani wiki nne; kati ya tarehe 6 Juni, 2023 na 2 Julai, 2023 mabasi ya kampuni ya New Force yamehusika katika ajali tano kama ifuatavyo:

| S/N | No.GARI | TAREHE YA TUKIO | MAHALI | MADHARA | CHANZO CHA AJALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | T171DZU<br><br>*(Saa 9.00 alfajiri)* | 06/06/2023 | Luanda-Mkoa wa Songwe | Majeruhi watu 2, uharibifu wa gari | Uzembe wa dereva wa basi T171DZU |
| 2 | T173DZU<br><br>*(Saa 9.00 alfajiri)* | 21/06/2023 | Igando-Mkoa wa Njombe | Vifo vya watu 7, majeruhi 48, uharibifu wa gari na miundombinu ya barabara | Uzembe wa dereva wa basi T173DZU |
| 3 | T742DFZ | 23/06/2023 | Mlandizi- Mkoa wa Pwani | Majeruhi na uharibu wa basi | Uzembe wa gari dogo na. T772DUX |
| 4 | T235DJQ<br><br>*(Saa 11.00 alfajiri)* | 25/06/2023 | Kitonga- Mkoa wa Iringa | Hakuna majeruhi, uharibifu mdogo wa basi | Uzembe wa dereva wa basi la New force |
| 5 | T448DDT<br><br>*(haikuwa na leseni ya LATRA)* | 02/07/2023 | Kitonga- Mkoa wa Iringa | Majeruhi na uharibifu wa gari | Uzembe wa dereva wa basi la New Force (Wrong overtaking) |

Uchunguzi wa awali uliofanywa na Mamlaka ulibaini kuwepo kwa uvunjaji wa makusudi wa Kanuni za Usafirishaji wa Magari ya Abiria, 2020 hususan kutumia ratiba za saa 9.00 alfajiri na saa 11.00 alfajiri bila dereva kuwa amethibitishwa na LATRA na pengine dereva kuwa amethibitishwa lakini hatumii mfumo wa utambuzi wa dereva (i-button) anapoendesha basi. Kanuni zinamtaka dereva anayeendesha basi la abiria kutumia kifaa cha utambuzi (i-button). Sharti hili tulianza kulitekeleza kwa madereva wa mabasi ya abiria yaliyopewa ratiba za kuanza safari 9.00 alfajiri na saa 11.00 alfajiri. Kampuni ya New Force ni miongoni mwa watoa huduma waliopewa ratiba za saa 09.00 alfajiri (mabasi 10) na saa 11.00 alfajiri (mabasi 28) ambapo walipewa sharti la kuhakikisha madereva watakaondesha mabasi kwa ratiba hizo ni wale waliothibitishwa na LATRA na kupatiwa ibutton kisha wawe wanatumia kifaa hicho ili tuweze kuwafuatilia kwa mfumo wetu wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS) yanapokuwa safarini.

Hata hivyo, uchunguzi tulioufanya kwenye magari haya yaliyopata ajali tumebaini ukikwaji wa sharti hilo kwa mabasi ya Kampuni ya New Force Enterprises. Kutokana na ukiukwaji huu, Mamlaka imeshindwa kuwatambua madereva waliokuwa wanaendesha mabasi haya ili kuweza kuwachukulia hatua au kupeleka taarifa zao Jeshi la Polisi – Kikosi cha Usalama Barabarani ili wawajibishwe kwa mujibu wa Sheria za Usalama Barabarani.

Aidha, tumebaini ukiukwaji wa ratiba za mabasi ambayo hayakuwa kwenye ratiba ya saa 9.00 alfajiri na saa 11.00 alfajiri kwa kufanya safari muda huo bila kibali cha LATRA. Jambo hili linasababisha ushindani usio na usawa kwenye sekta.

Hivyo basi, kwa mujibu wa kifungu cha 5(1)(b) na 6(b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, inayoipa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) jukumu la **kutoa, kuhuisha na kufuta vibali na lesesi za usafirishaji**; na **kukuza usalama wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na usalama wa watumiaji wa huduma za sekta zinazodhibitiwa**, kufuatia ukiukwaji huu na

mfulululizo wa matukio ya ajali kwenye kampuni ya New Force, **Mamlaka inafuta ratiba za 9.00 alfajiri na saa 11.00 alfajiri kwa mabasi yote 38 ya New Force Enteprises, ambapo mabasi 10 ni yale yanayoanza safari saa 9.00 alfajiri na mabasi 28 yanayoanza safari saa 11.00 alfajiri**. Hivyo, kuanzia tarehe 5 Julai, 2023, mabasi haya yatafanya safari zao kuanzia saa 12.00 asubuhi na kuendelea. Orodha ya mabasi 38 imeambatishwa kwenye taarifa hii. Hatua hii sio adhabu, na hatujasitisha leseni za mabasi haya, bali huu ni utaratibu wa kiudhibiti (regulatory measures) unaochukuliwa kwa lengo la kuhakikisha usalama wa abiria, chombo cha usafiri na mali. Ifahamike pia kwamba ni kosa kutoa huduma za usafiri wa umma bila kuwa na leseni ya LATRA.

Kwa upande mwingine, kumbukumbu zetu zinaonesha kwamba Mamlaka iliwahi kusitisha leseni za mabasi sita (6) ya New Force Enterprises katika miaka ya nyuma kutokana na madereva wake kukithiri katika ukiukwaji wa Sheria za Usalama Barabarani, na ilielekeza madereva wote wa Kampuni hii warudi darasani ambapo Kampuni ilitekeleza na kuwapeleka madereva hao Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT). Hapa tunaielekeza Kampuni kuwasilisha Orodha ya Madereva wake wote na namba zao za leseni. Mamlaka inaendelea kufanya uchunguzi kwenye menejimenti ya Kampuni ya New Force ili kufahamu wanavyoajiri madereva na kuwasimamia.

Kwa ujumla, Mamlaka ipo kuwasaidia wawekezaji hawa kukuza mitaji yao na kuendelea kutoa huduma hizi kwa ufanisi. Kwa kampuni hii na nyingine tulizorekebisha ratiba zao (Ally’s Star na Katarama Express), tutaendelea kufuatilia mwenendo wao barabarani na endapo watajirekebisha, tutawarejesha kwenye ratiba za saa 9.00 alfajiri na saa 11.00 alfajiri.

**Ratiba za Safari za Mabasi ya Mikoani kwa Saa 24**

Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akiahirisha Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 28 Juni, 2023, alitoa tamko la uamuzi wa Serikali kuruhusu mabasi kusafiri saa 24. Katika tamko hili alieleza **(ninanukuu)**:

> *Ili kutekeleza uamuzi huu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itashirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi hususan sekta ya Uchukuzi kuweka utaratibu utakaofuatwa na wamiliki na madereva wa mabasi ya abiria wenye nia ya kusafirisha abiria nyakati za usiku."* **(Mwisho wa Kunukuu)**

Kufuatia maelekezo haya ya Serikali yaliyotolewa na Mhe. Waziri Mkuu, LATRA itakuwa tayari kusimamia utaratibu utakaowekwa na *Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi hususan sekta ya Uchukuzi ili ufuatwe na wamiliki na madereva wa mabasi ya abiria wenye nia ya kusafirisha abiria nyakati za usiku.*

CPA Habibu J. S. Suluo
**MKURUGENZI MKUU**

## 1. ORODHA YA MABASI YA NEW FORCE ENTERPRISES

| S/N | Na. GARI | ROUTE | RATIBA |
|---|---|---|---|
| 1 | T171DZU | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 09.00 Alfajiri |
| 2 | T172DZU | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 3 | T173DZU | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 09.00 Alfajiri |
| 4 | T623DMG | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 11.00 Alfajiri |
| 5 | T713DPK | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 09.00 Alfajiri |
| 6 | T213DKB | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 7 | T501DFR | MWANZA (NYEGEZI) -SINGIDA via SHINYANGA | 09.00 Asubuhi |
| 8 | T251DYD | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 09.00 Alfajiri |
| 9 | T918DKA | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 10 | T247DYD | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SONGEA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 11 | T612DMG | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 11.00 Alfajiri |
| 12 | T208DPB | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - MBEYA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 13 | T153DKX | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SONGEA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 14 | T151DKX | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SONGEA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 15 | T717DPK | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 16 | T236EBK | DAR ES SALAAM(MAGUFULI BUS TERMINAL) - MBEYA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 17 | T232EBK | DAR ES SALAAM(MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 18 | T175DZU | DAR ES SALAAM(MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 09.00 Alfajiri |
| 19 | T613DMG | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 11.00 Alfajiri |
| 20 | T177DZU | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - | 09.00 Alfajiri |

| S/N | Na. GARI | ROUTE | RATIBA |
|---|---|---|---|
| | | TUNDUMA via MOROGORO | |
| 21 | T240EBK | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - MBEYA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 22 | T242EBK | DAR ES SALAAM(MAGUFULI BUS TERMINAL) - MBEYA via MOROGORO | 09.00 Alfajiri |
| 23 | T255DYD | DAR ES SALAAM(MAGUFULI BUS TERMINAL) - SONGEA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 24 | T618DMG | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 25 | T245DYD | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SONGEA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 26 | T232DJQ | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - KYELA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 28 | T744DFZ | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 09.00 Alfajiri |
| 29 | T208DKB | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - TUNDUMA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 30 | T346DLY | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - KYELA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 31 | T235DJQ | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - KYELA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 32 | T614DMG | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 11.00 Alfajiri |
| 33 | T257DYD | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - KYELA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 34 | T155DKX | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SONGEA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 35 | T152DKX | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SONGEA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 36 | T227DJQ | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - KYELA via MOROGORO | 11.00 Alfajiri |
| 37 | T623DMG | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 11.00 Alfajiri |
| 38 | T713DPK | DAR ES SALAAM (MAGUFULI BUS TERMINAL) - SUMBAWANGA via MBEYA | 09.00 Alfajiri |

## 2. MABASI YA NEW FORCE LIYOPATA AJALI HIVI KARIBUNI

| S/N | No.GARI | TAREHE YA TUKIO | MAHALI | MADHARA | CHANZO CHA AJALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | T171DZU<br><br>*(Saa 9.00 alfajiri)* | 06/06/2023 | Luanda-Mkoa wa Songwe | Majeruhi watu 2, uharibifu wa gari | Uzembe wa dereva wa basi T171DZU |
| 2 | T173DZU<br><br>*(Saa 9.00 alfajiri)* | 21/06/2023 | Igando-Mkoa wa Njombe | Vifo vya watu 7, majeruhi 48, uharibifu wa gari na miundombinu ya barabara | Uzembe wa dereva wa basi T173DZU |
| 3 | T742DFZ | 23/06/2023 | Mlandizi-Mkoa wa Pwani | Majeruhi na uharibu wa basi | Uzembe wa gari dogo na. T772DUX |
| 4 | T235DJQ<br><br>*(Saa 11.00 alfajiri)* | 25/06/2023 | Kitonga-Mkoa wa Iringa | Hakuna majeruhi, uharibifu mdogo wa basi | Uzembe wa dereva wa basi la New force |
| 5 | T448DDT<br><br>*(haikuwa na leseni ya LATRA)* | 02/07/2023 | Kitonga-Mkoa wa Iringa | Majeruhi na uharibifu wa gari | Uzembe wa dereva wa basi la New Force (Wrong overtaking) |

J.J. Kahatano
Kny: **MKURUGENZI MKUU**